

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI



S.L.P. 9121

DAR ES SALAM

Anuani ya Simu: "ELIMU"
DAR ES SALAM
Telex: 42741 Elimu Tz.
Simu: 110146/9, 110150/2
Fax: 113271

Unapojibu tafadhali taja:

Tarehe: 2 Mei, 2002

Kumb.Na. ED/OK/C.2//4/111/13

Makatibu Tawala wa Mkoa
Makatbu Tawala wa Wilaya
Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Kanda,
Wakuu wa Vyuo vya Ualimu
Wakuu wa Shule za Sekondari,
TANZANIA BARA.

WARAKA WA ELIMU NA. 11 WA MWAKA 2002

**KUANZISHA HUDUMA ZA MALEZI NA USHAURI NASAHA KWA
WANAFUNZI KATIKA SHULE NA VYUO VYA UALIMU**

Kukosekana kwa huduma thabiti ya malezi na ushauri nasaha katika shule na vyuo vyetu, kumwafanya vijana wetu kushindwa kukabiliana na mabadiliko ya haraka yanayotokea katika mazingira yao na duniani kwa ujumla. Hali hii imesababisha mmomonyoko wa maadili mema ya jamii.

Kasoro zilizojitokeza katika shule na Vyuo vya Ualimu ni pamoja na baadhi ya wanafunzi kuvunja sheria za shule/vyuo, utoro, kuharibu mali ya umma, kufanya makosa ya jinai, kujihusisha na matumizi ya madawa ya kulevya pombe na uasherati. Vitendo hivyo huhatarisha maisha yao ikiwa ni pamoja na kuambukizwa magonjwa ya zinaa na virusi vya UKIMWI.

Hali kadhalika tishio la athari za UKIMWI limesababisha kubaguliwa na kutengwa kwa vijana wa shule wanaoishi na virusi au walioathirika kwa sababu ya UKIMWI.

Wizara kwa kutambua kasoro hizi imeamua kuchukua hatua zinazostahili ili kudhibiti hali hii katika shule na vyo. Kwa hiyo, kuanzia sasa kila shule/chuo kitakuwa na kamati ya malezi na mwalimu wa malezi na ushauri.

Waraka huu unaanza kutumika tarehe 1 Julai 2002.

Umesainiwa

R.A. Mpama

KAMISHNA WA ELIMU

MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA UANZISHAJI WA HUDUMA ZA MALEZI NA USHAURI SHULENI

1. Kila Mkuu wa Shule/chuo anaagizwa ateue mwalimu mlezi ambaye ataratibu shughuli zote za malezi na ushauri nasaha kwa wanafunzi na walimu.
2. Mwalimu, mlezi apunguziwe vipindi vya kufundisha ili apate nafasi ya kutekeleza shughuli za malezi na ushauri. Apewe chumba cha kuwezesha kutekeleza wajibu wake.
3. Uchaguzi wa Mwalimu Mlezi.

Mwalimu Mlezi atachaguliwa na wanafunzi/wanachuo, walimu wote wakishirikiana na wajumbe wa Kamati ya Shule/Bodi ya Shule. Aidha, shule/vyuo vyenye wanafunzi mchanganyiko walezi wawili wa kike na kiume wachaguliwe ili kukidhi mahitaji ya jinsi zote.

4. Sifa za Mwalimu Mlezi

Mwalimu Mlezi awe na sifa zifuatazo: msikilizaji na mvumilivu, mwenye upendo na huruma, bidii ya kazi, mwaminifu na mtunza siri za wanafunzi/wanachuo; mpenda haki na mwenye moyo wa kutetea haki za wanafunzi/wanachuo; mwenye mahusiano na ushirikiano mzuri, awe karibu na wanafunzi/wanachuo, mwenye busara, awe hodari na jasi kuyakabili matatizo ya mwanafunzi/wanachuo/ walimu.

5. Kazi za Mwalimu Mlezi:

- Kuzungumza na wanafunzi kuhusu ukuaji wao na mabadiliko wanayopata katika miili yao kabla na baada ya kupevuka.
- Kufanya mkutano na wanafunzi/wanachuo ili kujadiliana kuhusu matatizo wanayokabiliana nayo kielimu, kiafya na kijamii na kuwasaidia kupata mbinu za kukabiliana na matatizo hayo.

- Kuwalinda na kuwatetea wanafunzi, wanachuo ili watendewe haki.
- Kushauriana na Mwalimu Mkuu/Mkuu wa Shule/Chuo, Walimu wa nidhamu na walimu wote kuhusu matatizo ya wanafunzi/wanachuo.
- Kuzungumza na wasichana ili kuwasaidia kupata mbinu za kukwepa kundi au marafiki wabaya.
- Kutoa ushauri nasaha kwa wanafunzi wote.

6. Wakuu wa Shule/Vyuo wanaagizwa kuunda Kamati ya Malezi na Ushauri Nasaha na Elimu dhidi ya UKIMWI. Kamati hii itakuwa ni Kamati ndogo ya Kamati ya Shule au Bodi ya Shule na itakuwa na wajumbe wafuatao:

- (i) Mwalimu Mlezi – katibu
- (ii) Mwalimu wa taaluma – Mjumbe
- (iii) Wawakilishi wawili wa walimu/wakufunzi
- (iv) Wajumbe kutoka mashirika ya dini – 2
- (v) Wananchi wanaokubalika kimalezi kutoka maeneo yanayozunguka shule/chuo (mwanamke 1, mwanaume 1) – 2.
- (vi) Wawakilishi wawili wa wanafunzi.
- (vii) Wajumbe watamchagua mwenyekiti kwenye kikao cha kwanza cha kamati hiyo.

7. Shughuli za Kamati ya Malezi na Ushauri na Elimu Dhidi ya UKIMWI zitakuwa kama ifuatavyo:

- Kuhimiza na kufuatilia shughuli za malezi na ushauri nasaha pamoja na ufundishaji wa elimu ya kujikinga na UKIMWI.
- Kuelimisha na kuhusisha jamii katika malezi na ushauri nasaha na elimu ya kujikinga na UKIMWI.
- Kumshauri Mkuu wa Shule/Chuo juu ya hali ya utoaji huduma za malezi na ushauri nasaha katika shule/chuo.
- Mkaguzi wa Kanda ataratibu shughuli zote za Malezi katika shule/vyuo katika Kanda yake.